HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA

FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE

SHULE YA SEKONDARI YA KIHESA,
S.L.P 214,
IRINGA

13/12/2020

KUMB. NA. KSS/IMC/JI/VOL.I/07
MWANAFUNZI……..
K.K……(MZAZI/MLEZI)

YAH: **MASHARTI YA KUJIUNGA NA SHULE -2021**

Awali ya yote, nachukua fursa hii kukupongezasana kwa kufaulu Mtihani wa Darasa la saba, hatakuweza kuchaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari ya Kihesa mwaka wa masomo **2021**
Nimatumaini yangu kwamba bahati hii utaitumia vizuri kwa **juhudi** na **maarifa** ya hali juu na kukuwezesha kufanikiwa katika masomo na shughuli nyingine muhimu kama vile uzalishaji mali, michezo n.k.
Aidha ni tegemeo letu kuwa, utaonesha **nidhamu** nzuri na utatekekeleza majukumu yako yote na kufuata sheria na kanuni mbalimbali za shule ikiwa ni pamoja na mashrti yote ya kujiunga na shule kama yalivyo ainishwa hapa chini

Shule ya sekondari ya Kihesa ni shule ya **Kutwa** na ni ya **mchanganiko.** Ipo katika **Manispaa ya Iringa,** jirani na Chuo Kikuu cha Iringa
Shule itafunguliwa siku ya Jumatatu ya tarehe **11/01/2021.** Mwanafunzi anatakiwa kufika siku hiyo Shule inapo funguliwa pamoja na Mzazi/Mlezi wake ili kukamilisha usajili wake.
Mwanafunzi aje na vitu vifuatavyo ili kukamilisha usajili;

a. Arudishe fomu ya ahadi ya mzazi na mwanafunzi.
b. Arudishe fomu ya uandikishaji pamoja na fomu ya Daktari.
c. Aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa.
d. Akabidhi Flat fail litakalokuwa limewekwa vitu vyote tajwa hapo juu (a-c)
e. Akabidhi Rimu moja ya karatasi, ufagio mmoja wa chelewa kama ilivyokubaliwa katika kikao cha wazazi cha tarehe 28/11/2019

Zaidi ninakutakia maandalizi mema na vilevile nakukaribisha wewe mwanafunzi pamoja na mzazi/mlezi katika shule ya Sekondari ya Kihesa.

……
MKUU WA SHULE KIHESA SEKONDARI
0677006169

MWONGOZO WA WANAFUNZI WA KIHESA SEKONDARI

A. SARE ZA SHULE

i. Wasichana wawe na blauzi mbili(2) nyeupe tetron mikono mifupi, sketi mbili(2)**ndefu** za kijani (code na. 22 au 23)
ii. Kwa Wavulana wawe na mashati mawili (2) meupe ya tetroni ya mikono mifupi na suruali mbili za kijani (code na. 22 au 23).

iii. Mwanafunzi awe na Tai mbili ndefu za kijani (rangi ya kitambaa cha sketi au suruali)
iv. Jozi mbili za viatu vyeusi vya kufunga na Kamba (visivyo na kisigino kirefu).
v. Jozi mbili za soksi nyeupe kwa wasichana na rangi yoyote kwa wavulana.
vi. Mwanafunzi awe na sweta moja la kijani mgomba lenye shingo ya "V"
vii. Kwa wasichana wa Kiislamu, wawe na Hijabu nyeupe, nusu kanzu nyeupe za tetroni na Suruali za kijani.
viii. Mwanafunzi awe na njum/raba, Bukta na flana (rangi nyekundu), traksuti kwa ajili ya michezo (rangi nyekundu).

NB. SARE ZINAZOBANA KWA WAVULANA NA SKETI FUPI KWA WASICHANA ZITACHANWA AU KUNYANG'ANYWA.

NB: (a) Hairuhusiwi kwa mwanafunzi yeyote kumiliki vifaa vifutavyo shuleni;
i. Simu, heleni, mikufu, shanga, bangili na radio.
ii. Kuwa na nywele ndefu.
iii. Kuvaa mavazi yaliyo nje ya sare ya shule.
(b) Mwanafunzi anapaswa kuwa katika sare ya shule
- wakati wa masomo darasani.
- Safari zote za nje na ndani ya shule kwa jina la shule
- Wakati wa kwenda Hospitali wakati wa shule.

B. VIFAA VYA DARASANI

Kila mwanafunzi anatakiwa awe na jumla ya daftari 10 (counter book quire 3) kwa ajili ya masomo ya darasani, Mkebe wenye vifaa vya kusomea Hisabati, kalamu (biki na penseli) na Begi imara la kubebea Daftari (counter book quire 3)

C. MIPAKA YA SHULE.

i. Unapaswa kufahamu mipaka ya shule na kutokutoka nje ya mipaka hiyo bila kibali maalumu, baada ya kufika shuleni.
ii. Ruhusa maalumu itatolewa na mwalimu wa darasa na kisha kupitishwa na mwalimu wa zamu kwa mwanafunzi mgonjwa au anayelazimika kuondoka shuleni kabla ya muda wa masomo kumalizika.
iii. Wanafunzi wasitembelee bila sababu ya msingi (a) Ukumbi wa Walimu (b) Ofisi za shule (c) Maabara
iv. Hairuhusiwi kabisa kwa mwanafunzi kutembelea
a) Vilabu vya Pombe b) Nyumba za starehe c) Nyumba za kufikia wageni

D. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

a) Wizi
b) Uvutaji sigara au bangi
c) Kuharibu kwa makusudi mali ya shule
d) Kuoa au kuolewa
e) Utoro wa shule wa muda mrefu
f) Uasherati
g) Makosa ya jinai
(h) kupata mimba
(i) kusababisha Mimba
(j) kupigana
(k) kudharau Bendera ya Taifa
(l) kutoa mimba
(m) utovu sugu wa nidhamu
(n) Ulevi wa aina yoyote

E. USAFI

Usafi ni wajibu wa kila mwanafunzi kama sehemu muhimu ya maisha yake ya kila siku, hivyo utashughulika
a) Usafi binafsi wa mwili na mavazi yako
b) Usafi wa maeneo yafuatayo kama utakavyopangiwa: vyoo, madarasa, maabara, viwanja na Barabara.

F. MENGINEYO

a) Mzazi wa mwanafunzi anayo haki ya kufuatilia mahudhurio, maendeleo, tabia na mwenendo wa mwanafunzi shuleni kwa kuwasiliana na Ofisi ya Mkuu wa Shule.
b) Wageni wa mwanafunzi wakati awapo shuleni ni lazima waonane kwanza na mwalimu wa zamu ambaye amepewa uwezo wa kukubali au kutokukubali kuonana na mwanafunzi.

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION
KIHESA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 214, IRINGA –TANZANIA

To be completed by the Medical officer.

Student's full name……
Age……..year……..Sex……..(M/F)
Blood Count Red and White cells……
Stool examination……
Urine analysis……
Syphilis test……
Eye test……
T.B test……
Ears……
Spleen……
Chest……
Abdomen……

ADDITIONA INFORMATION; e.g. Physical or chronical of family diseases, etc
……
……
……

I certify that, the above information filled are correct to my knowledge and the student is allowed/not allowed to continue with her/his studies.

Name and signature……..
Destination……
Section……..
Date……

NB; A student should bring this form dully by an authorized medical officer. No student will be registered if will not bring this form.

(Mwanafunzi anatakiwa kurudisha fomu hii baada ya kuwa imejazwa na daktari. Hakuna mwanafunzi atakayepokelewa na kusajilisha shuleni bila kuwa na fomu hii.)

WIZARA YA ELIMU ,SAYANSI NA TEKNOLOJIA
SHULE YA SEKONDARI YA KIHESA

FOMU YA KUKUBALI.

I. Sehemu hii ijazwe na mwanafunzi

1. Mimi…….(mwanafunzi) wa kidato cha ……..ninakubali kujiunga na shule ya sekondari ya Kihesa nikiwa mwanafunzi wa kutwa.
2. Ninakubaliana na masharti yote na nina ahidi kuwa, nitafuata sheria na taratibu zote za shule nikiwa kama mwanafunzi wa shule hii.
3. Niko tayari kuchukuliwa hatua mbalimbali za kinidhamu na uongozi wa shuleikiwa ni pamoja na kurudishwa kwa wazazi/walezi wangu endapo nitakiuka masharti na taratibu za shule kama zilivyo ainishwa katika fomu ya kujiunga na sahule.
4. Sahihi ya mwanafunzi…….....(isiwe ya mkorogo) tarehe……

II. Sehemu hii ijazwe na mzazi/mlezi

1. Mimi…… (Jina la mzazi/mlezi) nina kubali mwanangu/ndugu yangu……..wa kidato cha…….mwaka…....kujiunga na Shule ya Sekondari ya Kihesa kuanzia (tarehe) ……akiwa mwanafunzi wa kutwa.
2. Ninakubaliana na masharti na taratibu za shule kama zilivyo ainishwa katika fomu ya kujiunga na Shule.
3. Nitakuwa tayari kumpokea mtoto wakati wowote endapo atakiuka masharti yaliyobainishwa au kubainika kuwa na afya isiyoridhisha na ambayo inahitaji ukaribu wa mzazi/mlezi mwenyewe.
4. (a). Anwani yangu ya kudumu ni;

   ……
   ……
   Simu ya mkononi……..

   (b). Majina na anwani ya mlezi aliye karibu, ambaye shule inaweza kuwasiliana naye wakati wowote inapobidi kufanya hivyo:

	Jina la mzazi/mlezi	Uhusiano	anakoishi	mawasiliano
1.	……	……	……..	……
2.	……	……	……..	……
3.	……	……	……..	……

Sahihi ya mzazi/mlezi……. Tarehe……